# USAJILI WA WANAHABARI NA ATHARI ZAKE



Na Jenerali Ulimwengu

BARAZA LA
HABARI TANZANIA

© **Media Council of Tanzania, 2018**

Media Council of Tanzania
P.O.Box 10160,
Dar es Salaam.

**ISBN - xxxx**

## UTANGULIZI

Suala la iwapo wanahabari wasajiliwe ama la ni suala tata ambalo limekuwa likiwasumbua watunga-sera, watunga-sheria, wakuu wa serikali na wanahabari wenyewe kwa muda mrefu sasa. Kila moja katika makundi hayo linaliangalia suala hili kwa mtazamo wake tofauti.

Wakuu wa  serikali katika ngazi zote (wakuu wa kisiasa,, watumishi wa serikali, wabunge wa vyama-tawala) wanauona utaratibu wa usajili wa wanahabari kama jambo la kawaida kabisa, kwani ni kama haieleweki kwamba kundi muhimu la lawanataaluma linaweza likafanya kazi zake pasipo kusajiliwa ipasavyo.

Mtazamo kama huu hata hivyo unatiwa dosari na ukweli kwamba, pamoja na utetezi huu wa usajili wa wanahabari, upo ushahisi kwamba sheria nyingi zinazobainisha sababu ya kweli ya serikali kung'ang'ania usajili wa wanahabari, nayo ni utashi wa serikali kuidhibiti na kuibinya tasnia ya habari.

Hata baadhi ya wanahabari wamekuwa wakiikubali dhana hasi kuhusu 'uanataaluma.' Hoja imekuwa kwamba uandishi wa habari ni 'taaluma' kama taaluma nyingine kama vile udaktari, uhandisi na uanasheria, na kwa maana hiyo hawana budi kutendewa kama wengine wanavyotendewa.

Hoja hii inaonekana kuwa na mvuto wake kwa baadhi ya wanahabari, ambao wanaamini kwamba 'taaluma' yao inadhalilika kutokana na 'kuvamiwa' na watu wasiokuwa na elimu na stadi zinayotakiwa. Upo utashi wa wazi wa kuihami tasnia dhidi ya matendo ya baadhi ya watu wanaodai kuwa wanahabari bila kuwa na vigezo vinavyotakiwa.

Wanajamii kwa ujumla nao wamekuwa wakilalamika kuhusu watu wanaopita wakidai kuwa wanahabari lakini ambao ni vigumu kuwahakiki kuwa ni wanahabari wa kweli na ambao kazi zao mara nyingi ziko chini ya viwango. Mbaya zaidi, baadhi yao wamechukua taswira ya 'omba-omba,' wanaojialika kwenye matukio na kisha kuomba nauli za kurrejea majumbani kwao.

## USAJILI KWA AJILI GANI?

Hoja zote hizi zinazounga mono dhana ya usajili zina uzito fulani ambao hauna budi kutazamwa kwa makini. Mtazamo wa maofisa wa serikali (na wengine, ikiwa ni pamoja na wanahabari wenyewe) wanaodhani kwamba wanahabari wanana budi kusajiliwa kama wanataaluma wengine), angalau kwa mahitaji wa ulipaji kodi, wana mantiki kwa kiwango fulani.

Inaeleweka kwamba serikali lazima iwe na kiwango fulani cha taarifa kuhusu shughuli zote za kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni na kijamii zinazofanyika chini ya himaya yake, na hiyo ina maana kwamba makundi yote yanayohusika na shughuli hizi hayana budi kuwa ndani ya daftari moja au jingine kwa matakwa kama vile ya ulipaji kodi na mengine. Kimantiki, mahitaji kama hayo yatazihusu asasi za habari, lakini hayahusiki na usajili wa mwandishi mmoja mmoja.

BARAZA LA
HABARI TANZANIA

## Mwanahabari ni nani?

Hoja dhidi ya usajili wa wanahabari imejikita katika suala tata la nani anweza kuitwa mwanahabari. Suala hili limezua mjadala mgumu baina ya wanahabari wenyewe na pia miongoni mwa wanajamii.

Upo mtazamo unaomwangalia mwanahabari kama mtu aliye angalau na kiwango fulani cha elimu na ambaye na mbaye amepata mafunzo ya kiwango fulani cha stadi za kiuandishi zinazomwezesha kuripoti, kuhariri, kutangaza , kuandaa vipindi na kutengeneza programu na makala nyingine za vyombo vya habari. Kimapokeo, mtu kama huyu ni yule anayepokea mafunzo minajili ya kuwa mwajiriwa na gazeti, au kituo cha redio au televisheni.

Mtazamo tofauti na huu ni ule unaomwona mwanahabari kama mwanajamii ye yote ambaye anajishughulisha na utafutaji na usambazaji wa taarifa kuhusu masuala muhimu ndani ya jamii, na ambay anaweza kuwa amepitia mafunzo



mahsusi ya kiuandishi au la. Kinachohitajika kwa mwanajamii kama huyu ni uwezo wa kuelewa na kuzingatia anachokiona katika jamii na uwezo wa kutosha wa kukiwasilisha kwa wanajamii wengine.

Bila shaka, kutakuwa na uelewa unaotofautiana baina ya watu wanaoangalia masuala haya katika uhalisia unaotofautiana. Nafasi ya mpuliza-baragumu, ambayo imefifia kidogo katika zama zetu, ambayo jukumu lake lilikuwa ni kuitanabahisha jamii kuhusu wingu la nzige limalokitihia kijiji, au maporomoko ya ardhi yanayokaribia, nafasi hiyo haina budi kuchukuliwa kama uanahabari.

Ingawaje tunaweza kubeza taratibu hizo za kale kwa kuziona kama za kizamani mno na zilizopitwa na wakati, nafasi hiyo ya wahenga imechkuliwa na mkereketwa wa mitandao ya kijamii ambaye mara zote yuko na Twitter, Facebook, Whatsapp or kwenye blog yake binafsi akiutaarifu ulimwengu kuhusu lo lote atakalo. Ujio wa kile kinachoitwa 'raia-mwanahabari' umefanya hali iwe tata zaidi.

Katika vijiji vingi katika nchi za Kiafrika, ambako jamii nyingi hazijaendelea sana kutoka zilivyokuwa karne moja iliyopita, nafasi ya mwanahabari asiyelipwa na ye yote imebakia.






Malumbano kuhusu suala hili aghalabu husahau hata 'etimolojia' ya neno 'journalist' ambalo linatokana na neno la Kifaransa 'journal', ambalo sasa kina mana ya gazeti, lakini maana yake ya asili ni kumbukumbu binafsi za kila siku; katika utamaduni wa Wazungu, kila mtu anayo 'journal' yake binafsi ambamo huhifadhi mambo aliyoyafanya au kuyashuhudia, au mambo yaliyomtokea kwa siku husika ('diary')..

## Usajili ni nini, na una tofauti gani na uandikishaji kwa shughuli mahsusi, (Accreditation)?

Utaratibu wa usajili (Registration) wa wanahabari hutofautiana kutoka nchi moja hadi nyingine, lakini kwa ujumla sheria hutaka kwamba kila anayetaka kufanya kazi kama mwanahabari ajisajili na mamlaka husika, kwa kawaida wizara inayohusika na habari. Katika baadhi ya nchi, mwanahabari anatakiwa ahuishe (renew) usajili wake kila mwaka, na apewe 'press card' yenye namba ya mwaka aliosajiliwa na kuhalalishwa kama mwanahabari.

Upande wa pili wa sharti hili ni kwamba usajili huo unaweza kukataliwa mwanahabari anapokwenda kujisajili mwanzoni mwa mwaka, kama ambavyo sheria za baadhi ya nchi zinasema. Kwa maana hiyo, usajili wa lazima wa wanahabari unabeba mbegu za kuweza kumnyima kibali cha kufanya kazi kama mwanahabari yeyote anayeomba.

Uandikishaji mahsusi wa wanahabari kwa shughuli mahsusi (Accreditation) umekuwa ukiangaliwa kwa namna tofauti na usajili. Wanahabari kutoka nje ya nchi wanaweza kuandikishwa mahsusi kwa lengo la kuweza kufanya katika nchi iliyowapokea, wakati wanahabari wa ndani nao wakitakiwa kupata uandikishwaji mahsusi kwa ajili ya kuweza kuingia na kufanya kazi mahali mahsusi au kwa matukio mahsusi, kama vile Bunge, Ikulu, Mahakama au viunga vya michezo.

Uandikishaji kama huu unakuwa na umuhimu katika kudhibiti idadi ya wanahabari wanaoweza kuingia maeneo finyu, ambayo ni tofauti na kuwadhibiti wanahabari kupitia taratibu za usajili, ambazo zinaweza kutumiwa na mamangimeza wa serikali kuwaengua wanahabari 'wakorofi'.

Je, ipo toifauti ya msingi kati ya 'registration' na 'accreditation' katika muktadha mzima wa uhuru wa tasnia ya habari ? Mara nyingi maneno haya hutumika kwa kubadilishana, kama vile yana maana moja, lakini tofauti yake hujitokeza katika utekelezaji. Mara nyingi pia, hutegemea ni ofisa gani anakuwa langoni kwa muda husika.

Hapa lazima itambulike kwamba, katika hali ya madola ya Kiafrika, ambayo hayajaingia katika utawala wa kidemokrasi, tabia za watendaji wa umma si kutaka kusaidia uandishi wa habari bali ni kuubana kwa kila mbiu inayoweza kubuniwa.

Katika serikali zetu zote, uwepo wa wizara ya habari ni ukumbusho kwamba nchi zetu hazijaingia katika utaratibu wa kidemokrasia, kwani jukumu kuu la wizara hii ni udhibiti wa habari na kufanya propaganda, ambayo yanaweza kuhalalishwa tu katika hali mazingira ya vita.

BARAZA LA HABARI TANZANIA

## MIFANO YA SHERIA ZA USAJILI

Ziko nchi nyingi, hasa barani Afrika, ambazo zinazo sheria zinazotaka kila anayetaka kufanya kazi ya uandishi kuajiandikisha, na kuhuisha usajili wake kila mwaka. Kenya na Tanzania, kwa mfano, zinatoa mifano ya hivi karibuni ya serikali zilizotunga sheria za kulazimisha usajili wa wanahabari. Kenya imefanya hivyo kupitia Media Council (of Kenya) Act ya 2013, ambayo inalazimisha usajili wa wanahabari, biashara za habari na asasi za mafunzo ya uandishi.

Sababu zilizotamkwa za sheria hii ni kuboresha 'uanataaluma' kwa kuwafanya waandishi wanaofanya kazi nchini Kenya kuwa na stadi zinazohitajika. Hizo ndizo pia sababu zilizotolewa na wakuu wa serikali ya Tanzania wakati wakipitisha Sheria ya Huduma za Habari (MSA) ya mwaka 2016.

Tukiangalia MSA ya Tanzania, tunaona kwamba kuna kusudio la kuunda baraza la habari la kisheria ambalo litaisaidia serikali katika kuwadhibiti wanahabari, ikiwa ni pamoja na usajili na ina nyingine za udhibiti wa dola. Hili linafanyika leo, huku ikijulikana kwmaba lipo Baraza La Habari la Tanzania (MCT) lenye nguvu na ambalo limekuwa likisimamia utendaji katika tasnia ya habari, na ambalo limefanya kazi nzuri kiasi kwamba mfano wake umeigwa na nchi nyingine duniani.

Pengine si lazima kuingia katika undani wa shaeria hizi mbili (za Kenya na Tanzania), lakini ni muhimu kuzingatia baadhi ya vipengele vya sheria hizi. Kwa mfano, sheria zote mbili zinaweka ulazima wa kuwa na angalau kiwango cha chini kabisa cha elimu, shahada ama stashahada katika afni ya uanahabari. Pia sheria hizo zinaeleza kwamba mwombaji anaweza kukubaliwa ama kukataliwa, au aliyekuwa amekubaliwa anaweza kukataliwa anapokuja kuhuisha leseni yake/ kuandikisha upya.

Hoja ambayo imetolewa na maofisa wa dola, na wakati mwingine kuungwa mkono na baadhi ya wanahabari, ni kwamba viwango hivi bvya elimu vinalenga kuhakikisha kwamba waandishi wana viwango vya juu vitakavyowawezesha kufanya kazi

zao kwa weledi zaidi. Wanahabari wanaokubaliana na mtazamo huu wanaweza kuwa wanashawishika na hatua inayoonekana kama inayorejesha 'heshima ya taaluma' katika tasnia ya habari. Hata hivyo, watakuwa hawaangalii vyema vipengele vinavyominya uhuru wa kujieleza katika sheria hizi.

## UZOEFU WA AFRIKA KUSINI

Afrika kKusini ni mojawapo ya nchi za Afrika ambazo hazina sheria inayolazimisha usajili. Hata hivyo, tangu kupatikana kwa utwala wa demokrasia nchini humo mwaka 1994, kumekuwapo na mjadala mrefu kuhusu suala la usajili, pande nyingi zikisigana kuhusu suala hilo.

Mwaka 2012, Baraza la Habari la nchi hiyo liliamua kufanya utafiti kuhusu jinsi ya kuendesha shughuli za usimamizi wa tasnia ya habari, iwapo wananchi wanaridhishwa na utendaji wa bara la habari; iwapo uendeshaji wa mfumo wa kutosajili wanahabari umesaidia kuongeza uwajibikaji wa wanahabari; na kuangalia nchi za nje zinavyolichukulia suala zima la usajili wa wanahabari.

Idara ya Sayansi ya Mawasiliano ya Chuo Kikuu cha Afrika Kusini (UNISA) ndiyo iliopewa kandarasi ya kufanya kazi hiyo. Malumbano yalikuwa makali nchini wakati wa utafiti ho, hususan wawakilishi wa chama-tawala, ANC, wakidai kwamba zilihitajika hatua madhubuti zaidi za kusimamia tasnia ya habari huku wadau wengie wakipingahatua kama hizo.

Katika utafiti linganifu, wachunguzi walidurusu uzoefu wan chi za nje na wakagundua mwelekeo kwammba nchi zenye usimamizi unaofanywa na tasnia yenyewe (voluntary regulation) zina unafuu katika viwango vya ubora wa uhuru wa habari. Miongoni mwa nchi 50 zenye ubora wa juu kabisa katika kuheshimu huhuru wa habari, asilimia 70 ni zile zenye usimamizi wa tasnia yenyewe. Hizi ni takwimu zinazotolewa na Reporters Without Borders na Freedom House, ambayo

ndiyo mashirika makuu duniani yanayoaminika katika utoaji wa viwango vya ubora katika uheshimi wa uhuru wa habari katika nchi zote zza dunia.

Utafiti huo uligundua kwamba miongoni mwa nchi 16 bora kabisa duniani katika uheshimu wa uhuru wa habari, 15 zinao utaratibu wa usiammaizi wa rasnia yenyewe (self-regulation). Denmark kwa sasa imetoka kwa sababu ya matatizo yta kiuendeshaji, lakini kimsingi ni mojawapo ya hizo nyingine, na imesisitiza kwamba usimamizi wa tasnia ya habari nchini Denmark unafanyika nje kabisa ya udhibiti wa serikali ya nchi hiyo.

## MAONI

Haya hapa chini ni baadhi ya maoni (ya wataalamu pamoja na asasi) yanayoliangalia suala la usajili wa wanahabari, ambayo yanatoa mwanga zaidi kuhusu suala linalojadiliwa. Wanataaluma wenye maoni kama haya wapo wengi, na asasi zenye maoni kama haya zipo nyingi vile vile, ila hii ni mifano michache ambayo kiujumla inaunga mkono hoja ya kuwa na uendershaji wa usimamizi wa hiari (voluntary regulation).:


## Toby Mendel

Toby Mendel ni Mkurugenzi wa Sheria katika Article 19 na Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Demcrasia, nchini Canada. Mendel anatambua tofauti ambazo zimejitokeza kbaina ya mifumo mbali mbali ya usajili na uandikishaji wa wanahabari katika nchi nyingi. Mara kadhaa, amneno kama 'registration' na 'accreditation' yametumika kana kwamba yana maana ile ile, na hili linaweza kusababisha mikanganyiko. Anapendelea kutumia maneno 'licensing schemes' au mifumo ya utoaji leseni kuelezea mifumo yote mbali mbali ya utoaji wa vibali vya kazi kwa ajili ya wanahabari.

Anasema, 'ingawaje maelezo yanayotolewa kuhusu umuhimu wa kusajili wanahabari ni kwamba ni jitihada za kuhakikisha

kuwa wanahabari wanafanaya kazi kwa weledi mkubwa zaidi, lakini katika utekelezaji wake, mamlaka ya kutoa leseni yanaweza kuwa nyenzo ya kisiasa inayotumika kuwazuia wanahabari wakosoaji au wanahabari huru wasiandike. Kwa sababu hii, na kwa sababu haki ya kujieleza katika vyombo vya habari ni ya kila mtu bila kujali umahiri wake au uadilifu wake, mifumo yo yote ya usajili wa wanahabari ni kuingilia uhuru wa habari'.

## Stephen Strasser



Katika makala yake, 'Usajili wa Maripota: Jinsi Usajili wa Waandishi Unavyotishia Vyombo Huru vya Habari', Stephen Strasser, ambaye ni profesa mshiriki katika City University ya New York, anasema kwamba huko nyuma, zama za 'Vita Baridi,'

'Utoaji wa leseni kwa wanahabari ulikuwa na ladha ya kiitikadi, ilikuwa ni njia ya kuwaorodhesha waandishi katika harakati za ujenzi wa taifa.' Anaeleza kwamba katika hali mpya ya kisiasa iliyozuka baada ya anguko la Sovieti, dola zitaendelea kutaka kusajili wanahabari kwa nia tofauti, lakini nguvu inayotaka kuwepo na nafasi pana zaidi ya haki za binadamu na uhuru wa kujieleza inakuwa zaidi na zaidi.

Hata hivyo, anasita kutoa malekezo ya moja kwa moja kuhusu mfumo unaofaa kwa watu wote, na anatoa hadhari kuwa watu wawe waangalifu. Kwa mfano anauliza iwapo ingekuwa busara kuilaumu Rwanda (serikali) kwa matendo yake dhidi ya uhuru wa habari wakati tunaijua fika historia ya nchi hiyo.

Anapendekeza kwmaba wanahabari wajisimamie wenyewe; jamii iunganishe uhuru wa kujieleza na vyombo huru vya habari; upatikanaji wa ujuzi mkubwa zaidi katika tasnia ya habari kuliko mafunzo ya kinadhariaepke yake.

Strasser anamalizia kwa kusema:' Hakuna shaka kubwa kwamba waendeshaji wa wakuu wa tasnia ya habari na watetezi wa haki za binadamu hawana budi kupinga usajili wa wanahabari; wanahabari hawana budi kuhofia serikali yo yote inayotaka kuwawekea mizingo na kuwadhibiti....

## Mahakama ya Marekani ya Haki za Binadamu (IACtHR)

Mahakama ya Marekani ya haki za Binadamu (IACTHR) inayoshughulikia Marekani za Kaskazini na Kusini) ilitoa maoni yake mwaka 1985, na kusema kwmaba ilikuwa ni kosa kulinganisha wanahbari na taaluma nyingine kama uwakili au uganga.

Katika kesi iliyokuja mbele ya mahakama hiyo, serikali ya Costa Rica ilijaribu kutoa hoja kwamba, matakwa ya sheria ya nchi hiyo kwamba wanahabari wote wawe wanachama wa 'colegio' au chama cha waandishi, yalikuwa matakwa ya kawaida kwani yalilenga kuweka na nidhamu katika shughuli za umma, kwamba hatua hiyo ingeinua viwango vya uandishi na maadili na pia inegwalinda wanahabari dhidi ya wamiliki wa vyombo vya habari.

Mahakama iliamua kwamb uhuru wa kutafuta, kupokea na kusambaza habari ulikuwa umelindwa mahsusi kama haki ya binadamu, tofauti na taaluma nyingine. Mahakama ilizikataa hoja za serikali, na ikasisitiza kwamba, pamoja na hatua zo zote ambazo serikali ingependa kuchukua ili kuweka nidhamu katika shughuli za umma, haitakiwi kuingilia haki ya binadamu ya kimsingi ya uhuru wa habari kama sheria ya kutoa leseni ingefanya.

Hoja kwamba ilikuwa muhimu kuikinga tasnia dhidi ya

uandishi wa hovyo ilikataliwa kwa msingi kwmaba haki ya uhuru wa kujieleza haitakiwi kuwekewa mizingo, ambayo huku ikonekana kuwa ya msaada, ndiyo inayoua kile inachodai inataka kukilinda.

## Mahakama Kuu Zambia

Vyombo vingine vya kitaifa na kimataifa vimekuwa na mitazamo kama hii. Kwa mfano, mwaka 1997, Mahakama Kuu ya Zambia ilitengua jaribio la kuweka chombo cha kisheria cha kudhibiti wanahabari, na mahakama ikasema kwamba jaribio lo lote la kutoa leseni kwa wanahabari lingekorofisha uhuru wa kujieleza, bila kujali njia zinazotumiwa na jaribio hilo.

## Jumuiya ya Kimataifa

Mwaka 2004, vyombo vikuu vya kimataifa vinavyosimamia uhsu wa kujieleza, (UN Special Rapporteur on Freedom of Opinion and Expression; OSCE Representative on Freedom of the Media na OAS Special Rapporteur on Freedom of Expression) vilitoa tamko la pamoja lililosema kwamba 'wanahabari mmoja mmoja hawatakiwi kupewa leseni wala kujisajili.'

## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

Ni halali kutamka kwamba mjadala huu utaendelea kuwa na utata wake. Wapo wanaoamini kwamba wanahabari wanahitaji kuwekewa utaratibu wa udhibiti kwa njia ambayo itawafanya wanahabari watekeleze majukumu yao kwa weledi mkubwa zaidi na kwa kuzingatia maadili ya kazi zao, na kwamba hii ni pamoja na aina fulani ya usajli.

Mtazamo huu unadai kwmaba uanahabari hauna budi kuwa 'professional' kama vile zilizvyo taaluma nyingine kama zilzivyo taaluma za uwakili au uganga. Mtazamo unawahusisha hata baadhi ya wanahabari wanaodhani

kwamba wanadhalilishwa kwa kuwa ndani ya tasnia isiyokuwa na 'muhuri' wa kitaaluma kama wenzao.

Lakini upande mwingine umekuwa ukisisitiza kwamba uanahabari, pamoja na sekta nzima ya mawasiliano, ni sehemu muhimi nay a msingi ya haki za binadamu, kwani uwezo wa kuwasiliana ni miongoni mwa haki za msingi kabisa kwa sababu ndiyo haki ambayo juu yake hujengekea au kutekelezeka haki nyingine za binadamu. Bila uwezo wa kujieleza, bila shaka haiwezekani hata kutetea haki zako nyingine wala kuwafanya wanajamii wenzako wajue matatizo yakeo.

Kati ya makundi haya, liko kundi jingine ambalo liko tayari kuchukua mtazamo wa kadri, hata kama kwa kawaida wanapingana na mfumo wa utoaji wa leseni au usajili wa wanahabari. Mtazamo huu ungependa kwamba pale inapobidi kuwa na usajili kwa sababu mahsusi, basi usajili huo ufanyike baada ya kuwa kigezo cha 'ncha tatu' ('three-part test'), ndiyo kusema kwamba hatua inayochukuliwa inafuata sheria ya bunge; kwamba zuio linalowekwa ni kwa manufaa ya umma, na kwamba hatua yo yote inayochukuliwa inalingana na tatizo linalokusudiwa kutatuliwa.

Tunaweza kufanya majumuisho machache na kutoa mapendekezo:

- Uanahabari, ambayo ni nguzo ya kati katika mjengo wa haki za binadamu. ni haki ya kila mtu bila zuio lo lote.
- Uhuru huu haupaswi kuingiliwa na idara za dola au maofisa wa serikali isipokuwa katika mazingira yasiyokuwa ya kawaida kabisa, kwa mfano, vita.
- Kuingiliw ahuko hakuna budi kufuata 'three-part test' kam ilivyoainishwa hapo juu.
- Serikali na maofisa wa dola hawawezi kuaminiwa kusimamia utendaji wa vyombo vya habari kwa sababu vyombo hivyo ndivyo 'whistle-blower' na maovu mengi yanayolalamikiwa huanzia katika vyombo hivyo hivyo vya dola.

- Serikali ndicho chanzo kikuu cha maovu makuu yanayoitesa jamii , ufisadi na ukandamizaji wa haki za binadamu, na kwa jinsi hii, serikali haiwezi kuwa ndiyo inasimamia kazi ya whiste-blower dhidi ya serikali yenyewe.
- Usimmamizi wa hiari (self-regulation) usisitizwe kadri inavyowezekana. Utaratibu wa usimamizi wa hiari unaposhindikana, au maamuzi ya utaratibu huu yasipowaridhisha wahusika wa upande wo wote, bado wanayo haki ya kufuata mkondo wa haki mahakamani. Lengo liwe, kwa kadri tunavyoweza, kuondokana na imla ya maofisa na mamangimeza wa serkali. .
- Deomkrasia, ama kile kidogo tulichoweza kukusanya kwa taabu katika miongo miwili iliyopita, inachechemea ikirudi nyuma. Maeneo ya wanajamii kujiamulia mambo yao wenyewe yanaporwa, na serikali siku zote zitang'ang'ania dhamira yake ya kudhibiti tasnia ya habari ili kuzima sauti za wanaolalamikia udhalimu. Wakati huu, tasnia ya habari na asasi za kiraia hazina budi kufunga kibwebwe kwa ajili ya mapambano makali ziaid kupitia vyombo vya habari.

Ili vyombo vya habari vinusurike na vishamiri, havina budi kujsafisha, kuendeleza na kuboresha mafunzo ya kufyundi na kimaadili, kuhalikisha vinatoa huduma bora kabisa kwa jamii. Jamii inayopata huduma bora inazostahili kutokana na tasnia ya habari inayojali uhuru wa jamii yake ndilo kimbilio la vyombo vya habari wakati vikiwa vinashambuliwa.



**Media Council of Tanzania**


**Publised by Media Council of Tanzania (MCT)**
**P.O.Box 10160, Dar es Salaam, Tanzania**
**Tel: +255 22 2775728/2771947**
**Mob: +255-784314880 Fax +255 22 2700370**
**E-mail: medial@mct.or.tz Website: www.mct.or.tz**